

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA MJI WA NZEGA



TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KITUO CHA AFYA ZOGOLO

Imeandaliwa na:

Ofisi ya Mkurugenzi Mji,
S.L.P 256,
NZEGA.

JANUARI, 2018

**TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS. 500,000,000 KWA
AJILI YA UKARABATI NA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KITUO CHA AFYA
ZOGOLO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.**

1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Mji wa Nzega ni moja kati ya Halmashauri 8 (nane) za Mkoa wa Tabora ambapo kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Halmashauri ya Mji ilikuwa na wakazi **87,860**, kati yao wanaume ni **42,555** na wanawake **45,305**. Aidha, kwa mujibu wa maoteo ya mwaka 2017 Halmashauri ya Mji inakadiriwa kuwa na wakazi **99,405**. Halmashauri ya Mji wa Nzega ina Tarafa 1, Kata 10, vijiji 21, vitongoji 174 na Jimbo moja la Uchaguzi la Nzega Mjini.

Kutokana na pendekezo la kuigawa Wilaya ya Nzega kuwa na Halmashauri mbili yaani, Halmashauri ya Mji wa Nzega na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kwa mujibu wa toleo la nne la tarehe **5/08/2003** hivyo Halmashauri ya Mji wa Nzega ina eneo la Kilometa za Mraba **690.579** sawa na asilimia **0.9** ya Mkoa wa Tabora wenye eneo la Kilometa za mraba **76,151**.

**2.0 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KWA AJILI YA UKARABATI NA
UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KITUO CHA AFYA ZOGOLO**

Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji ilipokea jumla ya fedha kiasi cha **Tshs 500,000,000** tarehe 29/08/2017 kutoka ofisi ya Rais-TAMISEMI chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia (World Bank) kwa ajili ya utekelezaji wa Ukarabati na Ujenzi wa Miundombinu ya Kituo cha Afya Zogolo kilichoko Kijiji cha Zogolo Kata ya Nzega Ndogo.

Hata hivyo Halmashauri ya Mji wa Nzega ilipokea barua yenye Kumb Na . **AD.296/303/01/1/70** ya tarehe **16/08/2017** kutoka ofisi ya Rais-TAMISEMI inayohusu Ukarabati na Ujenzi wa Vituo ya Afya pamoja na kuisitiza kuwa lengo la Serikali ni Kuboresha na Kusogeza huduma za afya karibu zaidi na Wananchi hususani katika eneo la huduma za upasuaji kwa kinamama wajawazito, Hivyo Serikali imetoa maelekezo ya Matumizi ya fedha hizi kwa ajili ya ukarabati wa Miundombinu ya kituo cha Afya Zogolo kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa jengo la Upasuaji (Theatre)
- Ujenzi wa wodi ya Kina Mama na Watoto
- Ujenzi wa Nyumba moja ya Mtumishi inayojitegemea
- Ujenzi wa Maabara
- Ujenzi wa jengo la kuhifadhia Maiti
- Ujenzi wa Kichomea Taka

Aidha Halmashauri ilipokea barua yenye **Kumb.Na. AD.296/303/01/1/82** ya tarehe **21/09/2017** kutoka Ofisi ya Rais –TAMISEMI ambayo ilielekeza na kushauri matumizi ya “**FORCE ACCOUNT**” kwa mujibu wa kanuni ya 167 ya ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 kwa ajili ya kupunguza gharama za ujenzi pamoja na kuangalia ubora wa thamani ya kazi (value for money). Pia Barua ilisisitiza uundaji wa kamati mbalimbali kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa kazi na kuhakikisha malengo yanafikiwa, Kamati zilizoshauriwa kuundwa ni pamoja na Kamati ya Manunuzi, Kamati ya Mapokezi na Kamati ya Ujenzi. Kamati zote tatu ziliundwa na mapendekezo yake ya wajumbe wa kamati yalipitishwa katika kikao cha kamati ya Fedha kilichofanyika tarehe **29/09/2017**.

3.0 HALI YA UTEKELEAJI WA MRADI

Ukarabati na Ujenzi wa Miundombinu ya Kituo cha afya Zogolo ulianza tarehe **18/10/2017** kwa kutumia Mafundi wenyeji ambao wamefanya kazi chini ya usimamizi wa Mhandisi wa Halmashauri ya Mji.

Halmashauri imehusika na Ununuzi wa Vifaa na kuwapa Mafundi wenyeji kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zifuatazo.

- Ukamilishaji wa jengo la Upasuaji (Theatre)
- Ujenzi wa wodi ya Kina Mama na Watoto
- Ukamilishaji wa Nyumba moja ya Mtumishi inayojitegemea
- Ujenzi wa Maabara
- Ujenzi wa jengo la kuhifadha Maiti na Ujenzi wa Kichomea Taka

Hadi sasa Majengo hayo yamefikia kwenye hatua zifuatazo

- **Ukamilishaji wa jengo la Upasuaji (Theatre)**

Jengo la upasuaji limekamilika.

Ukamilishaji wa jengo hili umegharimu jumla ya **Tshs 121,412,900**.

Picha ya jengo la upasuaji katika hatua ya kuezeka



Picha ya jengo la upasuaji baada ya ukamilishaji upande wa mbele



Picha ya jengo la upasuaji baada ya ukamilishaji upande wa nyuma



Picha ya chumba cha upasuaji na mfumo wa gesi



- **Ujenzi wa wodi ya Kina Mama na Watoto**

Jengo la wodi ya kina mama na watoto limekamilika na umegharimu jumla ya
Tshs 107,499,100.00

Picha ya wodi ya akina mama na watoto sehemu ya nyuma



Picha ya wodi ya akina mama na watoto sehemu ya ndani



- **Ukamilishaji wa Nyumba moja ya Mtumishi inayojitegemea**

Umaliziaji wa nyumba moja ya mtumishi inayojitegemea umekamilika na umegharimu jumla ya **Tshs 72,750,000.00**

Picha ya nyumba ya mtumishi kabla ya ukamilishaji



Picha ya nyumba ya mtumishi baada ya ukamilishaji



- **Ujenzi wa Maabara**

Ujenzi wa jengo la maabara umekamilika na umegharimu jumla ya **Tshs 75,400,000.**

Picha ya maabara katika hatua ya upauaji



Picha ya maabara iliyokamilika



- **Ujenzi wa jengo la kuhifadhia Maiti**

Jengo limekamilika ujenzi huu umegharimu jumla ya Tshs 18,089,100

Picha ya jengo la kuhifadhia maiti



- **Ujenzi wa Kichomea Taka**

Jengo limekamilika ujenzi huu umegharimu jumla ya Tshs 4,622,500

Picha ya kichomea taka



Hadi sasa ujenzi wa miradi yote iliyoagizwa na Serikali umegharimu jumla ya **Tshs 399,773,600.00**. Aidha kiasi cha fedha jumla ya **Tshs 100,226,400.00** ambacho kimebakia jumla ya **Tshs 95,236,000.00** zimetumika kufanya ukarabati wa majengo ya zamani na kiasi cha **Tshs 4,990,400.00** kimebaki

katika akaunti kwa ajili ya marekebisho madogo madogo ya jengo la upasuaji(Theatre).

Miradi ya zamani iliyofanyiwa ukarabati ni kama ifuatavyo:-

- **Wodi ya Wanaume na Wanawake,**

Ukarabati wa wodi ya wanaume/wanawake/watoto na bima umegharimu jumla ya **Tshs 18,564,000.00**

Picha ya wodi ya wanaume na wanawake iliyokarabatiwa



- **Nyumba sita (6) za Watumishi,**

Ukarabati wa nyumba sita za watumishi umegharimu jumla ya **Tshs 42,701,000.00.**

Picha ya moja ya nyumba za watumishi kabla ya ukarabati



Picha ya moja ya nyumba za watumishi iliyokarabatiwa



- **Ujenzi wa nyumba ya kufulia nguo (Laundry),**
Ujenzi wa nyumba ya kufulia nguo (laundry) upo usawa wa lenta na umegharimu jumla ya **Tshs 9,745,000.**

Picha ya nyumba ya kufulia nguo (Laundry)



- **Ukarabati na ujenzi wa njia za Kupitia Wagonjwa (Walk ways)**

Ujenzi wa njia za kupitia wagonjwa (Walk ways) umegharimu jumla ya

Tshs 16,145,000.00

Picha ya njia za wagonjwa(Walk ways)



- **Ukarabati wa vyoo vya Wagonjwa.**

Ukarabati wa vyoo vya wagonjwa umekamilika na umegharimu jumla ya

Tshs 6,761,000.0

Picha za vyoo vya wagonjwa vilivyokarabatiwa



- **Ukarabati wa jiko**

Ukarabati wa jiko umegharimu jumla ya **Tshs 500,000.00**

Picha ya jiko lililokarabatiwa



- **Ukarabati wa vyoo vya wodi**

Ukarabati wa vyoo vya wodi umegharimu jumla ya **Tshs 400,000.00**



- **Upakaji rangi bati OPD**

Upakaji rangi bati OPD umegharimu jumla ya **Tshs 420,000.00**

Picha ya OPD kabla ya ukarabati



Picha ya OPD iliyopakwa rangi



4.0 MAJENGO YANAYOHITAJI FEDHA KWA AJILI YA UKAMILISHAJI

- Ujenzi wa jengo la kufulia (laundry) unahitaji jumla ya **Tshs 11,739,660** kwa ajili ya ukamilishaji.
- Ujenzi wa njia za wagonjwa (Walk ways) unahitaji jumla ya **Tshs 7,580,660** kwa ajili ya ukamilishaji.
- Ujenzi wa vyoo unahitaji jumla ya **Tshs 3,000,000** kwa ajili ya ukamilishaji.
Halmashauri ya Mji wa Nzega inahitaji jumla ya **Tshs 22,320,320** kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo yaliyobaki katika Kituo cha Afya Zogolo.

Nawasilisha

Philemon M. Magesa
**MKURUGENZI MJI
NZEGA.**